SEHEMU YA TATU

UWEZO WA MUNGU WA KUENEZA INJILI ULIMWENGUNI.

LENGO: KUHAKIKISHA TWAENEZA INJILI KWA NGUVU ZA ROHO MTAKATIFU WALA SI KWA AKILI NA NGUVU ZETU BINAFSI.

1. YESU ALIWAITA WAFUASI WAKE WAENEZEE INJILI ULIMWENGUNI LAKINI AKAWAONYA WASIENDE, HADI WAPOKEE UWEZO WAKE MUNGU.

A. Maandiko katika Luka 24:46-49 kuhusu 'Utenzi mkuu" wa Yesu baada ya yeye kusema kwamba maondoleo ya dhambi yapaswa kufanywa katika jina lake, kwa mataifa, Yesu akawaambia wanafunzi wake wangojee hadi wajazwe nguvu za Mungu.

"Nami mwenyewe nitawapelekeeni yule ambaye Baba aliahidi kumtuma, lakini ngojeni huku mjini mpaka mtakapopewa ile nguvu ya juu." Luka 24:49.

B. Kisha katika matendo 1:8, Yesu alisema kwamba ratiba yao ya kueneza injili itakuwa:
   1. Nguvu za Mungu kwanza.
   2. Kisha kushuhudia kwa ulimwengu wote.

   "Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapowashukieni ninyi, mtajazwa nguvu na mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, katika nchi yote ya Yudea na Samaria, hata kwenya mipaka yote ya dunia." Matendo 1:8.

C. Baadaye wafuasi wa Yesu, wanaume na wanawake mia moja ishirini walikusanyika pamoja kwa siku kumi kusali (Matendo 1:14) wote wakajazwa na Roho Mtakatifu. (Matendo 2:4)

II ROHO MTAKATIFU ALIWAFANYIA NINI WALE WA KWANZA WALIOTUMWA KUUELEZA ULIMWENGU KUHUSU YESU?

A. Aliwapa nguvu za kazi ya Mungu kwa sababu Yesu alijua hawangeweza kuwa mashahidi kwa nguvu na uwezo wao wa kibinadamu.
   1. Matendo 11:22-24 yasema, Mungu alipomtumia Barnaba kuwaleta maelfu ya watu kwa Bwana, alikuwa amejazwa Roho Mtakatifu.

   2. Paulo alisema, zilikuwa nguvu zake Mungu zilizofanya kazi kwa uwezo mkubwa ndani yake.

      "Kwa madhumuni hayo, mimi nafanya kazi na kujitahidi nikizitumia nguvu kuu za kristo zifanyazo kazi ndani yangu." Wakolosai 1:29.

   3. Paulo alijua kwamba siyo maneno yake yaliyomwezesha kutenda aliyotenda, bali zilikuwa nguvu za Roho Mtakatifu.

      "Maana tulipowahubirieni ile Habari njema, haikuwa kwa maneno tu, bali pia kwa nguvu na kwa Roho Mtakatifu tukiwa na hakika kwamba ujumbe huo ulikuwa wa kweli." 1 Watesalonike 1:5.

   4. Paulo alipokabiliana na maovu makuu, na mchawi huyo akapofushwa (Matendo 13:8-11), nguvu za Paulo zilitokana na Roho Mtakatifu aliyekuwa amejaa ndani yake.

B. Roho Mtakatifu aliwapa wafuasi wa Yesu ujasiri wa kuhubiri neno la Yesu - hata alipokuwa akiwahubiria wale walimsulubisha Yesu. (Matendo 2:14-23).

C. Ujasiri wa kustahimili taabu na hata kufa kwa ajili ya Yesu ulitokana na Roho Mtakatifu.

III MBONA WAKRISTO LEO WAHITAJI NGUVU KAMA HIZO ZA ROHO MTAKATIFU TUNAPOJITAHIDI KUKAMILISHA KAZI YA KUENEZA INJILI ULIMWENGUNI KOTE KWA NIABA YA YESU.

A. Ni kweli kwamba kila mtu anayempokea Yesu kuwa mwokozi, hupokea Roho Mtakatifu wakati huo - kama Petero alivyouambia umati wa watu alipokuwa akihubiri siku ya pentekoste.

"Tubuni na kila mmoja wenu abatizwe katika jina la Yesu Kristo ili mpate kuondolewa dhambi zenu na kupokea ile zawadi ya Roho Mtakatifu." Matendo 2:38.

B. Walakini, ipo kazi nyingi ya Roho Mtakatifu inayoendelea hivi kwamba Wakristo waihitaji katika kueneza neno la Yesu ulimwenguni kote.

1. Ijapokuwa Mungu ni mwenyezi na huweza kufanya chochote, Waefeso 3:20 hutuambia kwamba anaweza tu kufanya mambo hayo makubwa kulingana na nguvu zifanyazo kazi ndani yetu.

"Kwake yeye ambaye kwa nguvu zake zifanyazo kazi ndani yetu, aweza kufanya mambo makuu zaidi ya yale tuwezayo kuomba au kufikiria."

2. Basi kwa kujaribu kueneza injili kwa nguvu zetu wenyewe badala ya kumwacha Mungu afanye kazi kupitia kwa Roho Mtakatifu, twapunguza yale Mungu aweza kufanya kupitia ndani yetu.

3. Paulo alisali katika Waefeso 1:18-19 kwa Wakristo ambao tayari walikuwa na Roho Mtakatifu ndani yao:

*"Mpate kutambua jinsi uwezo wake ulivyo **MKUU** mno kwa ajili yetu sisi tuaminio."*

C. Mbona nguvu za kibinadamu hazitoshi katika kueneza injili?

1. Mipango na ratiba si mbaya, lakini nguvu za Mungu kupitia Roho Mtakatifu ndizo zinazoweza kuwahukumu, kushawishi na kuwaleta watu kwa Yesu.

"Hotuba zangu na mahubiri yangu sikuyatoa kwa maneno ya kuvutia na ya hekima, bali kwa uthibitisho mwingi na nguvu za Roho Mtakatifu." 1Wakorinto 2:4

2. Kinyume cha uwezo hafifu wa kibinadamu, tunazo nguvu kama hizo zifanyazo kazi ndani yetu ambazo Mungu alizitia wakati alimfufua (Kristo) kutoka wafu na kumketisha kulia kwake mbinguni. Waefeso 1:19-23.

D. Kupungukiwa kwetu kwingi kwa ujasiri, na uhodari ni kwa sababu hatujitoi kwa yale Roho Mtakatifu ataka kutupatia tunapomwomba Mungu katika sala, na kumngojea atukabidhi.

IV WAKRISTO WAWEZAJE KUZUIA KAZI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA JUHUDI ZAO ZA KUENEZA INJILI ULIMWENGUNI?

A. Kwa kuzima Roho Mtakatifu (kwa kuuzima moto wake)
"Msipinge Roho Mtakatifu." 1 Watesalonike 5:19.

1. Wakristo huzima Roho wa Mungu kwa kutumia mipango na ratiba za kibinadamu, badala ya nguvu za mwenyezi Mungu kufanya kazi ndani yao.

   "Kwa nje wataonekana kama watu wenye kumcha Mungu, lakini wataikana nguvu yake ..." 11 Timoteo 3:5.

2. Pia twamzima kwa kujaribu kushawishi kwa maneno yetu ya busara na utaratibu badala ya kumtegemea Roho Mtakatifu kuonyesha nguvu zake kupitia neno lake na sala. (1 Wakorinto 2:4-5).

3. Twamzima Roho Mtakatifu kwa kupuuza himizo la Roho Mtakatifu anapotutuma kumhubiria mtu aliyepotea anayejua yuko tayari kusikia kuhusu Yesu.

4. Kwa kuwa na wasi wasi kuwahubiria watu kwa njia yako mwenyewe na katika wakati wako, wakati Roho wa Mungu hajakamilisha kunyoosha mioyo yao na kuwavuta, pia huzima uwezo wa Roho Mtakatifu.

5. Kwa kutojitoa kikamilifu kwa nguvu zake, twapunguza uwezo wa Mungu katika kutoweza kwake kufanya maajabu na makubwa yake kwa niaba ya Yesu.

B. Kwa kumhuzunisha Roho Mtakatifu.
"Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu." Waefeso 4:30.

1. Wakristo wamhuzunisha Roho Mtakatifu kwa dhambi zilizo maishani mwao, wakizuia nguvu zake kutiririka kupitia ndani yao.

2. Tazama "hakuna dhambi isiyoungamwa katika maisha ya mwombaji" katika sehemu ya 2 ya matayarisho yetu ya kibinafsi, ujue la kufanya kuhusu dhambi zako kama Mkristo ili usimhuzunishe Roho Mtakatifu.

3. "Usimhuzunishe Roho Mtakatifu" iko kati kati ya orodha ya vitu ambavyo Wakristo wapasa kufanya na kutofanya ili kuepukana na kutenda dhambi katika Waefeso 4:25-32.

V. TWAWEZAJE KUHAKIKISHIWA KWAMBA TUTAKUWA NA ROHO MTAKATIFU TUNAPOSHUHUDIA NA KUHUBIRI NENO LA YESU ULIMWENGUNI?

A. Tubu na uziache dhambi zo zote zinazomhuzunisha Roho Mtakatifu.
B. Hakikisha kuwa hatumzimi kwa kusisitiza kufanya vitu kwa njia zetu wenyewe.
C. Amini Waefeso 5:18 kwamba ni nia ya Mungu kwa sisi Wakristo ambao ndio tuliandikiwa hii, na ambao tulipokea Roho Mtakatifu tulipookolewa, tuendelee kujazwa na Roho Mtakatifu. (Ngeli katika Kigriki inaendelea, ni utaratibu unaoendelea).

D. Amini ahadi ya Yesu katika Luka 11:13.

"Ninyi ingawa ni waovu, mwajua kuwapa watoto wenu vitu vizuri. Basi Baba yenu wa mbinguni atafanya zaidi, atawapa Roho Mtakatifu wale wanaomwomba."

E. Uwe tayari kuwa peke yako na Mungu katika sala kabla ya kushuhudia, ukijiondolea tamaa yako na kumwomba nguvu na busara yake - ili ujazwe na Roho mtakatifu wa Mungu badala ya nafsi yako.

MAZOEZI

1. Chunguza neno la Mungu kwa moyo wazi ili upate maagizo yake kwako binafsi kuhusu Roho Mtakatifu.
2. Tazama kwa makini njia na matokeo ya vile unavyoshuhudia. Je, Mungu ana mengi zaidi kwako.

SALA YAKO

1. Tubu dhambi zo zote zinazomhuzunisha na kumzima Roho Mtakatifu, na uziache.
2. Sasa mwombe Roho Mtakatifu wa Mungu akujaze busara, ujasiri na nguvu ambazo anajua wazihitaji kuweza kuendeleza injili.
3. Kwa unyamavu, mngojee akupe uwezo, nguvu na ujasiri.